Informed consent

Swahili

Ridhaa katika huduma za afya

Ni nini maana ya ridhaa katika huduma za afya?

Huduma za afya zitakusaidia wakati una tatizo la ugonjwa au afya. Wakati mwingine unahitaji vipimo vya afya au matibabu. Mfanyakazi wa afya lazima akuulize kama unakubaliana kufanyiwa vipimo au matibabu. Ridhaa ni wakati umeelewa wazi tatizo la ugonjwa au afya yako na kukubaliana na kile mfanyakazi wako wa afya anachokwenda kufanya.

Unapaswa kufahamu kuhusu uchaguzi wako wote wa huduma za afya kabla ya kukubaliana. Unaweza kuchagua kupata matibabu au kukataa.

Ni habari gani ninazozihitaji?

Mfanyakazi wako wa afya atakupasha habari ya kukusaidia kufanya uamuzi kuhusu vipimo vyako au matibabu.

Unaweza pia kuuliza mfanyakazi wako wa afya maswali kama:

- » Nina ugojwa gani au nina tatizo gani la afya?
- » Ni kipimo gani au matibabu?
- » Ni namna gani kipimo au matibabu yatanisaidia?
- » Je kipimo au matibabu yanaweza kusababisha tatizo lolote?
- » Ni kwa kiasi gani tatizo linaweza kuleta madahara?
- » Je kuna aina mbalimbali za vipimo au matibabu?
- » Je ni nini kitafanyika baada ya vipimo au matibabu?
- » Je nitapata unafuu?
- » Je itachukua mda gani kupona?
- » Itatokea nini kama sitapata matibabu?

Mwambie mfanyakazi wako wa serikali kama kuna kitu ambacho hauelewi.

Kwa nini nalazimika kutoa ruhusa?

Katika Australia, ni sheria kwamba mfanyakazi wako wa afya lazima apate idhini yako kabla ya kutoa vipimo au matibabu.

Kwa nini nahitaji kutia sahihi fomu ya idhini?

Utaulizwa kutia sahihi fomu ya ridhaa iliyoandikwa kwa ajili ya matibabu hatari kama upasuaji. Mara nyingine unahitajika kuwaambia mfanyakazi wako wa afya kwamba unakubaliana. Ni wafanyakazi tu wa afya wanaoshiriki katika vipimo vyako na matibabu wataosoma fomu ya idhini yako.

Fomu yako ya ridhaa haitachangiwa na mtu yeyote asiyeshiriki katika huduma ya afya yako.

Nani anatoa ruhusa?

Kama unaweza kuelewa chaguzi za matibabu yako na unaweza kuwaambia mfanyakazi wako ni afya gani unataka, basi unaweza kuwa mtu wa lazima kuamua. Unaweza kuwaleta marafiki, familia au wanajamii katika miadi yako na kuwaomba ushauri. Wakati mwingine mfanyakazi wako wa afya, familia au rafiki wanaweza kufanya maamuzi kwa ajili yenu katika wakati wa dharura.



Nani anatoa ruhusa kwa mtoto?

Kwa kawaida, mzazi, mwangalizi au mlezi hutoa idhini kwa mtoto chini ya umri wa miaka 18. Kama mtoto anaweza kuelewa matibabu yao na athari anazoweza kuzipata juu ya afya yake, wanaweza kutoa ridhaa. Mfanyakazi wa afya ataangalia kama mtoto ana uwezo wa kutoa idhini yake mwenyewe.

Ni nahitaji kufahamu kwa kiasi gani?

Mfanyakazi wa afya atakupa habari zaidi kama unataka. Watajaribu kujibu maswali yako yote. Mwambie mfanyakazi wako wa afya kama kuna kitu chochote hauhitaji kujua kuhusu vipimo vyako au matibabu.

Ninahitaji mda mgani wa kuamua?

Maamuzi yanahitajika haraka wakati wa dharura. Kama si dharura, unaweza kuchukua muda zaidi wa kuamua. Kama bado hauna uhakika juu ya vipimo vyako au matibabu, unaweza kuzungumza na mfanyakazi wa afya mwingine ili kukusaidia kufanya uamuzi wako.



Je ninahitaji mkalimani?

Inaweza kuwa vigumu kuelewa vipimo vya afya au matibabu. Kufanya maamuzi bora, ni muhimu wewe na mfanyakazi wako wa afya kuelewa kila mmoja. Kama Kiingereza sio lugha yako ya kwanza, mkalimani mwenye utaalamu anaweza kuhudhuria miadi yako. Wakalimani wa uso kwa uso au wakalimani wa simu ni wa bure. Wewe au mfanyakazi wako wa afya anaweza kuomba mkalimani ili akae nanyi wakati wa majadiliano juu ya huduma ya afya yako. Taarifa unamwelezea mkalimani wako zitawekwa kwa usiri binafsi.

Inakuwaje kama nikitoa kibali na kisha mimi kubadili mawazo yangu?

Daima unaweza kubadili akili yako, hata kama umetia sahihi fomu ya idhini au ulimwambia mfanyakazi wako wa afya kuwa unakubaliana na vipimo au matibabu.

Kumbuka

Kuuliza maswali

Ni muhimu kuelewa kila kitu ambacho mfanyakazi wako wa afya amekuambia. Unaweza kuuliza maswali mengi unayoyataka. Unaweza kuleta mtu mwingine wa kukusaidia.

Omba mkalimani

Wakalimani wenye utaalamu ni wa bure. Wanarahisisha kwa wewe na mfanyakazi wako wa afya kuelewana.

♦ Ni chaguo lako

Hata kama ukitoa ruhusa, unaweza kubadilisha mawazo yako mda wowote.



Partnering with Consumers - This patient information brochure supports National Safety and Quality Health Service Standard 2 (2.4.1) Consumers and/or carers provided feedback on this patient information.

This document has been reproduced with the permission of Metro South Hospital and Health Service.

Swahili informed consent Effective: 10/2016